**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

# HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS MHESHIMIWA HARUSI SAID SULEIMAN (MBM) KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**MEI, 2023**

YALIYOMO

A. UTANGULIZI........................................................... 1
B. MUUNDO NA MAJUKUMU YA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS ........................................................ 2
C. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU MAKUU YA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA KIPINDI CHA JULAI 2022 – MACHI 2023 ......................................... 4
Ukusanyaji wa Mapato ........................................................ 4
Changamoto na Mafanikio.................................................... 5
Mapato na Matumizi ya Kawaida ........................................... 8
D. UTEKELEZAJI WA MIRADI INAYOSIMAMIWA NA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA KIPINDI CHA JULAI 2022 – MACHI 2023 ............... 9
Fedha za Maendeleo ........................................................... 9
Utekelezaji wa Miradi ya Mazingira...................................... 10
E. UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MAFUNGU YA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA KIPINDI CHA JULAI 2022 – MACHI 2023 ......................... 11
UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS ........................................................ 11
FUNGU B04 – MAMLAKA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA........................................................... 12
Programu ya Usimamizi wa Mazingira .................................. 12
Programu ya Utumishi na Uendeshaji ................................... 13
FUNGU C04 – MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBA NA NA DAWA ZA KULEVYA ........................................... 14
Programu ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya........................... 14
Programu ya Utawala na Rasilimali watu.............................. 17

FUNGU C05 – TUME YA UKIMWI .................................... 18
Programu ya Kuratibu Muitiko wa Taifa wa UKIMWI.......... 18
Programu ya Uratibu na Uendeshaji wa Tume ya UKIMWI.. 21
UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA OFISI KUU – FUNGU B01 ........................................................................ 22
Programu ya Usimamizi wa Mazingira na Uratibu wa Mabadiliko ya Tabianchi ........................................................ 23
Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Watu wenye Ulemavu................................................................ 23
Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ................................................... 25
F. MWELEKEO WA BAJETI KWA MAFUNGU YA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA MWAKA 2023/2024 ............................................... 31
MWELEKEO WA BAJETI KWA TAASISI ZA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS.............................. 31
FUNGU B04 MAMLAKA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA.......................................................... 31
FUNGU C04 MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBA NA NA DAWA ZA KULEVYA ........................................ 32
FUNGU C05 TUME YA UKIMWI ...................................... 33
MWELEKEO WA BAJETI YA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS ................................................ 35
MWELEKEO WA MATUMIZI KWA PROGRAMU ZA OFISI KUU – FUNGU B01 .................................................. 36
i. Programu ya Usimamizi wa Mazingira na Uratibu wa Mabadiliko ya Tabianchi ............................................. 36
ii. Programu ya Watu wenye Ulemavu; na ............................ 36
iii. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Makamu wa

Kwanza wa Rais............................................................................ 36
Programu ya Usimamizi wa Mazingira na Uratibu wa Mabadiliko ya Tabianchi.......................................................... 36
Programu Kuu ya Watu wenye Ulemavu................................ 38
Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ........................................................... 38
G. SHUKURANI ........................................................................ 42
H. HITIMISHO............................................................................ 43
Kiambatanisho nam. 1(a): Muhtasari wa Upatikanaji wa Fedha Julai - Machi 2022/2023 (000)..................................... 48
Kiambatanisho nam. 3: Makusanyo ya Mapato kwa Julai-Machi 2022/2023 na Makadirio ya 2023/2024.............. 55
Kiambatanisho nam. 4: Fedha za Miradi ya Mazingira......... 56
Kiambatanisho 5: Maeneo ya Kimazingira na Mashimo yaliyokaguliwa...................................................... 58
Kiambatanisho nam. 6 Idadi ya Watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais................................................ 60
Kiambanisho nam. 7 Idadi ya Visaidizi Vilivyogaiwa........... 63

# HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS

# MHESHIMIWA HARUSI SAID SULEIMAN (MBM) KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kutujaalia neema ya uhai, afya njema na uwezo wa kukutana hapa leo kwa lengo la kujadili utekelezaji wa majukumu yetu kwa kipindi cha mwaka 2022/2023 na kuweka mwelekeo wa mwaka wa fedha 2023/2024 kwa dhamira ya kuendelea kuwatumikia wananchi wote wa Zanzibar.

2. **Mheshimiwa Spika,** pongezi za dhati kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuendelea kuimarisha uchumi, umoja na mshikamano imara kwa wananchi wote. Kadhalika, nawapongeza Makamu wa Kwanza wa Rais, Mheshimiwa Othman Masoud Othman kwa kusimamia vyema utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, kwa majukumu mbalimbali pamoja na mashirikiano yao kwa pamoja na jinsi wanavyomsaidia na kumshauri vyema Mheshimiwa Rais

katika kufanikisha majukumu ya kitaifa kwa ujumla. Kwa kweli wananchi tunaridhishwa na uongozi wao, Mwenyezi Mungu aendelee kuwabariki. Nakushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi pamoja na Wenyeviti wa Kamati na Wajumbe wa Baraza lako Tukufu na Watendaji wa Baraza la Wawakilishi, kwa kuendelea kushirikiana na sisi na kutuongoza katika kutekeleza vyema majukumu yetu.

3. **Mheshimiwa Spika,** baada ya shukurani hizo, naomba uniruhusu kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Taarifa hii imezingatia Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050; Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar 2021 – 2026; Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia 2030; Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2020 – 2025 na Hotuba za Mheshimiwa Rais kwa nyakati mbalimbali. Bajeti hii pia imezingatia malengo ya Mpango Mkakati wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa mwaka 2021 – 2026 na malengo ya Programu ya Kuirithisha Zanzibar ya Kijani kwa Mwaka 2022/2023 – 2027/2028.

## B. MUUNDO NA MAJUKUMU YA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS

4. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imeundwa na Idara na Taasisi zifuatazo:-

i. Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira;

ii. Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya;
iii. Tume ya UKIMWI;
iv. Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu;
v. Ofisi ya Faragha ya Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais;
vi. Idara ya Mazingira;
vii. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
viii. Idara ya Utumishi na Uendeshaji
ix. Ofisi Kuu Pemba

5. **Mheshimiwa Spika,** majukumu yanayosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ni: -

i. Kusimamia masuala ya uhifadhi, usimamizi na utunzaji wa mazingira na uratibu wa masuala ya mabadiliko ya tabianchi;
ii. Kudhibiti na kupambana na usafirishaji, usambazaji na utumiaji wa dawa za kulevya;
iii. Kuratibu na kusimamia masuala ya UKIMWI;
iv. Kusimamia na kuratibu masuala ya Watu Wenye Ulemavu;
v. Kuratibu mambo yote yanayohusu Ofisi ya Faragha ya Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais;
vi. Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa masuala yote ya kisera ya Ofisi wa Makamu wa Kwanza wa Rais na
vii. Kushughulikia uendeshaji na usimamizi wa rasilimali watu katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

## C. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU MAKUU YA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA KIPINDI CHA JULAI 2022 – MACHI 2023

**Ukusanyaji wa Mapato**

6. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inakusanya mapato kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira. Kwa mwaka 2022/2023, Ofisi ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 300,000,000.00 ambazo zinatokana na ada ya uhifadhi na ada ya ukaguzi wa mazingira ili kuchangia mapato ya Serikali. Kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023, jumla ya shilingi 224,500,000.00 zilipangwa kukusanywa. Hadi kufikia Machi 2023, jumla ya shilingi 242,975,400.00 ambazo ni sawa na asilimia 108 ya kiwango kilichopangwa zilikusanywa sawa na asilimia 81 ya kiwango cha mwaka. *Kiambatanisho nam. 3 kinahusika.*

7. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ilijiwekea malengo yafuatayo:-.
   i. Kushughulikia athari za kimazingira zilizosababishwa na mabadiliko ya tabianchi na kutayarisha Mpango wa Kuirithisha Zanzibar ya Kijani (Zanzibar Green Legacy Programme);
   ii. Kuimarisha Ushughulikiaji wa masuala ya Watu wenye Ulemavu;
   iii. Kutekeleza Sheria ya Dawa za Kulevya;

iv. Kuendelea kupiga vita UKIMWI kwa lengo la kuuondoa katika orodha ya magonjwa hatarishi;

v. Kuendelea kuelimisha jamii kuhusu uhifadhi wa mazingira, kujikinga na maambukizo mapya ya VVU; kushajihisha jamii kuwajali, kuwahudumia na kuwaendeleza Watu wenye Ulemavu na kuimarisha vita dhidi ya dawa za kulevya kwa kufanya kampeni katika ngazi mbali mbali, ikiwemo jamii; na

vi. Kuimarisha uratibu wa masuala yanayosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

**Changamoto na Mafanikio**

**8. Mheshimiwa Spika,** changamoto zinazoendelea kuikabili Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ni:-

i. Upungufu wa vyombo vya usafiri kwa ajili ya Ofisi Kuu pamoja na Taasisi zake zote;

ii. Ufinyu wa nafasi za Ofisi ambapo kwa upande wa Unguja, Ofisi Kuu ya Wizara, Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu, Idara ya Mazingira, Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, na Tume ya UKIMWI zinakabiliwa na changamoto hiyo. Changamoto hiyo ni kubwa zaidi kwa Tume ya UKIMWI ambayo itatumia kiasi kikubwa cha fedha zake za Matumizi Mengineyo kulipia kodi ya jengo la ofisi.

iii. Kwa upande wa Mamlaka ya Dawa za Kulevya jengo linalotumika sasa lina mapungufu makubwa

kulingana na matakwa ya Sheria nam. 8/2021 ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya. Mamlaka pia inakabiliwa na ukosefu wa vifaa vya operesheni, mwenendo usioridhisha wa ushughulikiaji wa kesi za dawa za kulevya na wananchi kuwa na muhali katika kufichua wahalifu wa dawa za kulevya.

9. **Mheshimiwa Spika,** mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa mpango na bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ni kama ifuatavyo:-

i. Ofisi imekamilisha uandaaji wa programu ya Urithi wa Kijani Zanzibar (Green Legacy Programme) ambapo programu hiyo imeshapitishwa na Baraza la Mapinduzi na imepangwa kuzinduliwa mwezi Mei 2023.

ii. Sheria Nam. 8/2021 inayoanzisha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya na Sheria Nam. 8/2022 iliyoanzisha Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu zimetungwa na kuanza kutumika. Vile vile, Kanuni za sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya zimekamilika na hivi sasa zipo katika hatua ya kuchapishwa. Kanuni za Sheria ya Watu Ulemavu zimepelekwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa hatua za mapitio ya mwisho.

iii. Rasimu ya Kanuni ya kusimamia biashara ya hewa ya kaboni (Carbon Trading) na rasimu ya Kanuni za bio-teknolojia zimetayarishwa na kuwasilishwa

kwa wadau kwa ajili ya kukusanya maoni. Kanuni hizo zitakamilishwa baada ya taratibu za kisheria kuwekwa sawa.

iv. Kuanzisha huduma za upataji nafuu kwa waraibu wa dawa za kulevya katika kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia Kidimni; kuanzisha kituo cha pamoja cha uendeshaji wa kesi zinazohusiana na uhalifu wa kupangwa (Transnational Organized Crime Unit), na kuendelea na ujenzi wa mradi wa kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia. Aidha, Ofisi imepata eneo la ekari 6 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia –Kangagani, Pemba.

v. Ofisi pia imewatia hatiani watuhumiwa 15 wa kesi za dawa za kulevya na kupewa adhabu mbali mbali hadi kutumikia kifungo cha maisha.

vi. Ofisi inajivunia kuimarika kwa uhusiano na Taasisi za Usimamizi wa Sheria.

vii. Ofisi kupitia Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu imetoa jumla ya visaidizi 852 Unguja na Pemba. Kwa upande wa Unguja jumla ya visaidizi 469 (wanawake 240 na wanaume 229) na kwa Pemba visaidizi 383 (wanawake 250 na wanaume 133) vimetolewa.

viii. Kukamilisha utafiti wa kuangalia viashiria vya matokeo kwa masuala ya VVU na UKIMWI ambapo matokeo ya Utafiti yanatarajiwa kutolewa mwishoni mwa mwaka 2023.

**Mapato na Matumizi ya Kawaida**

10. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inasimamia Mafungu manne ambayo ni Fungu B01, linalosimamiwa na Katibu Mkuu; Fungu B04 linalosimamiwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira, Fungu C04 linalosimamiwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya na Fungu C05 linalosimamiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya UKIMWI.

11. **Mheshimiwa Spika,** kupitia mafungu hayo, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais iliidhinishiwa shilingi 10,505,320,000.00 katika utekelezaji wa majukumu yake. Kati ya fedha hizo shilingi 3,692,949,000.00 zilitengwa kwa ajili ya mishahara, na shilingi 6,812,371,000.00 zilikuwa kwa ajili ya matumizi mengineyo. Fedha zilizotengwa kwa kipindi cha miezi tisa ni shilingi 7,689,249,485.00 zikiwemo shilingi 3,047,776,995.00 za mishahara, na shilingi 4,641,472,490.00 za matumizi mengineyo. Jumla ya fedha zilizopatikana ni shilingi 5,470,618,870.00 sawa na asilimia 71 zinazojumuisha shilingi 3,859,626,070.00 sawa na asilimia 127 kwa ajili ya mishahara na shilingi 1,610,992,800.00 sawa na asilimia 35 kwa matumizi mengineyo ikilinganishwa na kiasi kilichokadiriwa kutumika katika kipindi cha miezi tisa. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 54 ya jumla, asilimia 92 ya mishahara na asilimia 27 ya matumizi mengineyo kwa makadirio ya mwaka mzima. *Kiambatanisho nam. 1 kinahusika.*

## D. UTEKELEZAJI WA MIRADI INAYOSIMAMIWA NA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA KIPINDI CHA JULAI 2022 – MACHI 2023

### Fedha za Maendeleo

12. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inatekeleza miradi inayohusu Usimamizi wa Mazingira na Uratibu wa Mabadiliko ya Tabianchi.

13. **Mheshimiwa Spika,** jumla ya shilingi 5,914,646,863.00 zilitengwa kwa shughuli za maendeleo ambapo shilingi 4,500,000,000.00 za SMZ na shilingi 1,114,646,863.00 ni za Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2023, fedha za Washirika wa Maendeleo shilingi 526,844,603.00 sawa na asilimia 48 zilitumika kutekeleza programu ya Usimamizi wa Mazingira na Uratibu wa Mabadiliko ya Tabianchi. *Kiambatanisho nam. 4 kinahusika.*

### Utekelezaji wa Miradi ya Mazingira

14. **Mheshimiwa Spika,** kupitia Mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Maji Machafu katika eneo la Msingini – Kichungwani Chake Chake, Pemba, Ofisi imetoa mafunzo ya siku tano ya kitaalamu juu ya uendeshaji wa mtambo wa usafishaji maji machafu katika eneo la Msingini ambapo yaliwashirikisha watendaji wakuu wa mradi kutoka sekta ya Mazingira, Wakala wa Majengo, Baraza la Mji Chake Chake, Maabara ya Afya ya Jamii pamoja na ZAWA. Mradi huu pia,

umejenga msingi wa maji ya mvua wenye urefu wa mita 100 kwenye eneo la Mtoni Shehia ya Madungu kupitia Kampuni ya KINS.

15. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi kupitia Mradi wa Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa jamii za Pwani ya Zanzibar, imetoa mafunzo ya upandaji wa miti ya juu na mafunzo ya ufugaji endelevu wa nyuki katika maeneo ya mradi, Unguja na Pemba. Jumla ya washiriki 119 walipatiwa mafunzo hayo. Aidha, Ripoti za awali (baseline studies) za ufugaji nyuki na upandaji wa miti ya juu katika maeneo ya mradi zimetayarishwa.

16. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi pia imefanya utafiti wa kina juu ya athari za matumizi ya zana haramu kwa matumbawe yaliyomo kwenye eneo la hifadhi la Mkondo wa Pemba (PECCA). Utafiti huu umefanyika kupitia Mradi wa Kuimarisha Jamii kwa Kuzingatia Ikolojia na Shughuli za Kujipatia Kipato kwa Wavuvi Wadogo na Usimamizi wa Eneo la Hifadhi la Mkondo wa Pemba, PECCA. Vile vile, Ofisi kupitia mradi huu imetoa zana za uvuvi na vifaa vya doria kwa Kamati 11 za Uvuvi za Shehia kwenye eneo la Hifadhi ya Mkondo wa Pemba (PECCA). Kamati zilizonufaika ni Mbuyuni, Makombeni, Mizingani, Wambaa, Kilindi, Mgelema, Chonga, Ndagoni, Tibirinzi, Wesha na Shungi.

17. **Mheshimiwa Spika,** kupitia Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa Mfumo wa Ikolojia Vijijini

(EBARR), Ofisi imekamilisha uchimbaji wa visima sita, ujenzi wa minara ya kuhifadhia matangi ya maji pamoja na ufungaji wa “Solar panel” kwenye visima hivyo viliopo katika Shehia tatu za Matemwe Kijini, Mbuyutende na Jugakuu. Aidha, mradi unaendelea na ujenzi wa vituo vitatu vya wajasiriamali wa sabuni, vipodozi, ushoni na upakasaji pamoja na kituo cha huduma za mafunzo ya mifugo katika Shehia hizo.

## E. UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MAFUNGU YA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA KIPINDI CHA JULAI 2022 – MACHI 2023

### Utekelezaji wa Programu za Taasisi zinazosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais

### Fungu B04 – Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira

18. **Mheshimiwa Spika,** fungu hili linatekeleza Programu Kuu mbili ambazo ni Usimamizi wa Mazingira na Utumishi na Uendeshaji.

### Programu ya Usimamizi wa Mazingira

19. **Mheshimiwa Spika,** shughuli zilizotekelezwa kupitia programu ya usimamizi wa mazingira ni pamoja na kuendelea kusimamia upigaji marufuku mifuko ya plastiki kwa ajili ya kupunguza athari za kiafya na kimazingira zinazotokana na mifuko hiyo. Katika kipindi hiki operesheni

65 (24 Unguja na 41 Pemba) zimefanyika na watu 148 (98 Unguja na 50 Pemba) wakiwa na tani 6.4 (tani 4.2 Unguja na tani 2.2 Pemba) wamekamatwa na kutozwa faini ya shilingi 15,880,000.00 (shilingi 12,110,000.00 Unguja na shilingi 3,770,000.00 Pemba). Aidha, operesheni 48 za kusimamia maliasili zisizorejesheka zimefanyika (10 Unguja na 38 Pemba) ambapo gari saba za ng'ombe zilikamatwa Pemba na kutozwa faini ya jumla ya Shilingi 1,400,000.00. Misumeno minne ya moto (3 Unguja na 1 Pemba) na 'grander' mbili za kupasulia mbao zilikamatwa Pemba na kutaifishwa. Vile vile, korja 3.5 za mbao za mtondoo zilikamatwa katika Shehia ya Kilindi, Chake Chake zikiwa hazina kibali cha kupasuliwa kwa mashirikiano na Idara ya Misitu na kutozwa faini ya jumla ya shilingi 1,500,000.00.

20. **Mheshimiwa Spika,** katika kupunguza athari za uharibifu na uchafuzi wa mazingira, Ofisi imefanya ufuatiliaji wa maeneo 92 (58 Unguja na 34 Pemba) yenye athari mbali mbali za kimazingira na mashimo 106 (52 Unguja na 54 Pemba) ya mchanga, kifusi, mawe na matofali ya mawe. Kwenye ufuatiliaji huo miongozo ya kimazingira imetolewa ambayo imesaidia kupunguza uchafuzi na uharibifu wa mazingira wa maeneo hayo.

21. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha miradi ya kiuchumi na kimaendeleo inatekelezwa bila ya kuathiri mazingira, tathmini za kimazingira 123 (105 Unguja na 18 Pemba) zimefanyika. Vyeti vya aina tofauti vya kimazingira vimetolewa vikiambatana na masharti ya kimazingira

kwa miradi hiyo. Aidha, ziara za ufuatiliaji wa miradi ya kiuchumi zimefanyika katika miradi 141 (86 Unguja na 55 Pemba) ya hoteli. Ziara hizo zimeonesha kwamba kwa kiasi kikubwa miradi hiyo inatekeleza masharti ya kimazingira.

22. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imekuza uelewa na elimu ya uzingatiaji wa sheria, kanuni na miongozo ya kimazingira kwa jamii kupitia vipindi 9 (4 vya TV, 2 vya redio, na vipindi 3 vya mitandao ya kijamii). Aidha, Ofisi ilishiriki Maonesho ya Kitaifa ya Tamasha la Biashara lililofanyika katika viwanja vya Maisara Mjini Unguja na Maonesho ya Kilimo yaliyofanyika Kizimbani, Unguja. Jumla ya wananchi 780 walitembelea banda la sekta ya mazingira na kupatiwa elimu. Ofisi pia imetoa mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi 34 wa Chuo cha Utawala wa Umma juu ya Tathmini za Athari za Kimazingira.

**Programu ya Utumishi na Uendeshaji**

23. **Mheshimiwa Spika,** kupitia programu hii, Ofisi imewajengea uwezo watumishi 8 (5 Unguja na 3 Pemba) kwa mafunzo ya muda mrefu na 15 (7 Unguja na 8 Pemba) kwa mafunzo ya muda mfupi. Aidha, huduma za ofisi zimetolewa zikiwemo huduma za kimtandao, upatikanaji wa maji safi na salama, matengenezo madogo madogo ya ofisi pamoja na huduma za umeme. Vile vile, stahiki mbali mbali zimelipwa kwa watumishi zikiwemo stahiki za likizo na muda wa ziada wa kazi.

24. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira iliidhinishiwa jumla ya shilingi 1,149,528,730.00 ambapo shilingi 649,818,730.00 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 499,710,000.00 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2023, jumla ya shilingi 936,496,135.00, sawa na asilimia 81 zilipatikana, ambapo shilingi 762,289,535.00 sawa na asilimia 117 ni mshahara na shilingi 174,206,600.00 sawa na asilimia 35 kwa matumizi mengineyo, *Kiambatanisho nam. 1 kinahusika.*

**Fungu C04 – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya**

25. **Mheshimiwa Spika,** fungu hili linatekeleza Programu Kuu mbili ambazo ni Udhibiti wa Dawa za Kulevya na Utawala na Rasilimali Watu.

**Programu ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya**

26. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi kwa kushirikiana na Serikali ya Uingereza imeanzisha Kituo Jumuishi (Transnational Organized Crime Unit) kwa ajili ya kuongeza kasi ya ushughulikiaji wa kesi zinazohusu uhalifu wa kupangwa ikiwemo dawa za kulevya. Kituo hicho kimeshaanza kazi ambapo kinawashirikisha watendaji kutoka katika taasisi mbali mbali za ulinzi na usalama za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

27. **Mheshimiwa Spika,** katika kuendelea kupambana na uhalifu wa dawa za kulevya, jumla ya kesi 312 ziliripotiwa na kufanyiwa kazi katika ngazi mbali mbali za kisheria zikiwemo kesi 25 zilizopo kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), kesi 31 kwa Mkemia Mkuu wa Serikali, kesi 215 zimefunguliwa Mahakamani na kesi 41 zinaendelea na upelelezi katika Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya. Kesi hizo zinajumuisha watuhumiwa 316 (306 wanaume na 10 wanawake) Unguja na Pemba.

28. **Mheshimiwa Spika,** katika jitihada za kuhakikisha watuhumiwa wa dawa za kulevya wanachukuliwa hatua za kisheria, Ofisi kwa kushirikiana na Ofisi ya DPP imefungua jumla ya majalada 215 ya kesi za dawa za kulevya katika Mahakama kuu na Mahakama za Mikoa Unguja na Pemba. Kati ya majalada hayo, majalada 149 kesi zake zinaendelea mahakamani, majalada 18 watuhumiwa wake wameachiliwa huru na majalada 15 watuhumiwa wametiwa hatiani.

29. **Mheshimiwa Spika,** katika kukuza uelewa kwa jamii juu ya Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, nam. 8/2021 jumla ya vipindi 69 vya redio na televisheni vilirikodiwa na kurushwa hewani. Aidha, elimu hiyo ilitolewa kwa skuli 107 za msingi na sekondari zikiwemo za Serikali na za Binafsi kwa Unguja na Pemba. Jumla ya wanafunzi 6,314 na walimu 164 walifikiwa. Aidha, elimu ya Sheria ya Dawa za Kulevya imetolewa kwa Masheha wa Shehia zote za Wilaya saba

za Unguja ikiwa ni miongoni mwa hatua za kudhibiti matumizi na usambazaji wa dawa za kulevya.

30. **Mheshimiwa Spika,** jitihada za utoaji wa huduma za upataji nafuu zimeendelea kuimarishwa katika Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia kilichopo Kidimni ambapo tokea kufunguliwa jumla ya waraibu 186 wamepokelewa. Kati ya hao waraibu 40 wameruhusiwa baada ya kukamilisha huduma ya tiba, waraibu 35 wameondolewa kwa sababu mbali mbali, waraibu 60 wametoroka na 51 wanaendelea kupata huduma. Vile vile, waraibu 15 wameunganishwa na kupatiwa mafunzo ya ujasiriamali baada ya kupata matibabu. Aidha, nyumba nne za Upataji Nafuu kwa Unguja na Pemba zilipatiwa ruzuku ya shilingi 2,000,000.00 kila moja kwa lengo la kuzijengea mazingira bora ya kazi ili ziweze kukabiliana na changamoto mbali mbali.

31. **Mheshimiwa Spika,** vikao mbali mbali vya mapambano ya dawa za kulevya vikiwemo vikao vya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa vimefanyika kwa kushirikiana na wadau wa ndani na wa nje kama vile UNODC, Drug Enforcement Administration, British Borders, World Custom Organization na Basel Institute. Lengo la vikao hivyo ni kubadilishana uzoefu na kujadili kwa pamoja changamoto zinazokabili ushughulikiaji wa uhalifu wa dawa za kulevya na uhalifu unaofanana nao na kutafuta namna bora zaidi ya kuzitatua.

**Programu ya Utawala na Rasilimali watu**

32. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imewajengea uwezo watumishi 15 wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa kuwapatia mafunzo ya uchunguzi wa uhalifu wa dawa za kulevya na utambuzi wa kemikali; mafunzo ya ukusanyaji wa taarifa za kiintelijensia katika upelelezi wa vitendo vya uhalifu pamoja na mafunzo ya ukaguzi wa abiria na mizigo katika bandari na viwanja vya ndege. Aidha, huduma za ofisi zimetolewa zikiwemo huduma za kimtandao, upatikanaji wa maji safi na salama, matengenezo madogo madogo ya ofisi pamoja na huduma za umeme.

33. **Mheshimiwa Spika,** vikao kumi vimefanyika vikiwemo vikao vinne vya Bodi ya Zabuni, vikao vinne vya Kamati ya Uongozi na vikao viwili vya Kamati vya Ukaguzi wa Ndani. Aidha, stahiki mbali mbali zimelipwa kwa watumishi zikiwemo stahiki za likizo, msiba, muda wa ziada wa kazi na kugharamia huduma za usafiri.

34. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya iliidhinishiwa shilingi 964,498,747.00 kwa matumizi ya kawaida zikiwemo shilingi 265,125,020.00 za mishahara na shilingi 699,373,727.00 za matumizi mengineyo. Hadi Machi 2023 fedha zilizoingizwa ni shilingi 804,945,000.00 ambazo ni sawa na asilimia 83. Fedha zilizopatikana kwa ajili ya mishahara ni shilingi 499,273,000.00 sawa na asilimia

188 na shilingi 305,672,000.00 sawa na asilimia 44 kwa matumizi mengineyo. Aidha, Ofisi iliidhinishiwa shilingi 3,637,825,000.00 kwa matumizi ya kazi za maendeleo na hadi Machi 2023, fedha zilizoingizwa ni shilingi 700,000,000.00 sawa na asilimia 19. *Kiambatanisho nam. 1 kinahusika.*

**Fungu C05 – TUME YA UKIMWI**

35. **Mheshimiwa Spika,** fungu hili linatekeleza Programu Kuu mbili ambazo ni Kuratibu Muitiko wa Taifa wa UKIMWI na Uratibu na Uendeshaji wa Tume ya UKIMWI.

**Programu ya Kuratibu Muitiko wa Taifa wa UKIMWI**

36. **Mheshimiwa Spika,** Lengo la programu hili ni kuhakikisha maambukizo mapya ya Virusi vya UKIMWI yanapungua kila mwaka hadi kumalizika kabisa ifikapo mwaka 2030. Ofisi hii imeendelea kuratibu muitiko wa taifa wa UKIMWI nchini unaozishirikisha sekta zote. Jamii yetu ielewe kuwa tatizo la maambukizo ya Virusi vya UKIMWI bado lipo nchini na linaendelea kuathiri watu. Hadi kufikia Disemba 2022, jumla ya watu 8,975 wamesajiliwa katika kliniki za tiba ambapo mwaka jana wakati ninasoma bajeti kama hii, watu waliosajiliwa walikuwa 7,589. Takwimu hizi zinaonyesha kwamba kuna ongezeko la watu 1,386. Aidha, uzito wa maradhi unaendelea kuwaelemea wanawake kuliko wanaume kwani kati ya watu 8,975 walioambukizwa VVU, watu 6,074 ni wanawake sawa na asilimia 67.6 ambapo

wanaume ni 2,901, sawa na asilimia 32.3. Ili kukabiliana na hali hii, nachukua fursa hii kuziomba taasisi za serikali na zisizo za kiserikali kushiriki kikamilifu katika kuchukua hatua zitakazosaidia kulimaliza tatizo hili ndani ya visiwa vyetu ifikapo 2030.

37. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2022/23, Tanzania imefanya tena utafiti wa kuangalia vishiria vya matokeo kwa masuala ya VVU na UKIMWI (Tanzania HIV Impact Survey – THIS). Tume ya UKIMWI kwa kushirikiana na Tume ya Kudhibiti UKIMWI ya Tanzania Bara na Washirika wa Maendeleo ilishiriki kikamilifu katika kufanikisha utafiti huu. Matokeo ya utafiti yatasaidia kutuonyesha picha halisi ya wapi tumefika kitaifa katika mapambano dhidi ya UKIMWI na kusaidia katika kuandaa mipango madhubuti katika kukabiliana na tatizo hili.

38. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imeendelea kutoa taarifa na elimu za VVU na UKIMWI ili kukuza uelewa juu ya masuala ya VVU na UKIMWI kupitia mikutano, mabonanza, matukio mbali mbali ya kitaifa kama vile sherehe za Mapinduzi, Sikukuu ya Wakulima (sabasaba) na Siku ya Wanawake Duniani. Njia nyengine zilizotumika ni kupitia mashindano ya resi za ngalawa na chemsha bongo kwa wanafunzi, majarida, vipindi vya redio na televisheni na mitandao ya kijamii (instagram, facebook na youtube) na programu ya Radio ya ONGEA. Hadi kufikia 2023, jumla ya watu 5,677 walifikiwa na vipeperushi 17,713 vilisambazwa.

**39.** **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imeingiza kipengele cha masuala ya UKIMWI katika Muongozo wa Uandaaji wa Mapendekezo ya Miradi ya Maendeleo ili kuhakikisha kwamba maambukizo ya VVU yanadhibitiwa wakati wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo husika. Pia, imeandaa Muongozo wa Kuandaa Mipango ya UKIMWI katika miradi mikubwa ya maendeleo ambao utatumiwa na sekta mbali mbali ambazo zitatekeleza miradi kupitia Tume ya Mipango.

**40.** **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ilifanya maadhimisho ya siku ya UKIMWI duniani tarehe 1 Disemba 2022, ikiwa ujumbe wa mwaka huu ni "Toa huduma za UKIMWI kwa usawa". Mgeni Rasmi katika maadhimisho hayo alikuwa ni Makamu wa Kwanza wa Rais, Mheshimiwa Othman Masoud Othman.

**41.** **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imechapisha nakala 100 za Muongozo wa Uzingatiaji wa Masuala ya UKIMWI katika juhudi za kuhakikisha kwamba mapambano dhidi ya UKIMWI yanakuwa endelevu na pia hayana gharama kubwa. Watumiaji wa Muongozo huo ni sekta za Serikali, sekta zisizo za serikali, asasi za kiraia zikiwemo taasisi za kidini. Muongozo huo unawarahisisshia watumiaji kuandaa mipango ya VVU yenye tija katika maeneo yao.

**42.** **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imefanya mkutano wa uratibu kwa sekta za serikali 16 na mashirika ya umma 12 kwa lengo la kupokea ripoti za utekelezaji wa sekta hizo, kujadili

na kubadilishana uzoefu juu ya uzingatiaji na utekelezaji wa shughuli za UKIMWI sehemu za kazi. Aidha, imefanya mikutano ya uratibu iliyojumuisha wadau mbali mbali wa sekta za Serikali na asasi za kiraia kwa lengo la kuimarisha huduma za afya ya uzazi, katika vituo vya tiba na vituo vya huduma rafiki kwa vijana. Jumla ya watu 6,412 walipima hadi Septemba 2022, ambapo watu 318 waligundulika na maambukizo (244 wanaume na 74 wanawake). Jumla ya watu 368 walifanyiwa uchunguzi wa saratani ya mlango wa shingo ya kizazi 24 waligundulika na tatizo hilo katika kliniki za tiba. Ofisi imetoa elimu kwa Waendesha bodaboda 60 wa wilaya ya Chake-chake kisiwani Pemba juu ya tabia hatarishi kwa maambukizo ya VVU na kupiga vita vitendo vya udhalilishaji. Aidha, Ofisi imetoa elimu kwa shehia zenye mazingira hatarishi zaidi kwa maambukizo ya VVU Kisiwani Pemba zikiwemo Machomanne na Wara.

### Programu ya Uratibu na Uendeshaji wa Tume ya UKIMWI

43. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imegharamia mafunzo kwa watendaji watatu, mmoja kwa ngazi ya Shahada ya Pili katika fani ya Ufuatiliaji na wawili kwa Shahada ya Kwanza katika fani ya Manunuzi na Maendeleo ya Jamii. Ofisi imewapatia wafanyakazi mafunzo ya afya ili kuongeza ufanisi wa kazi. Ofisi pia imefanya vikao 7 vya Bodi ya Makamishna, Bodi ya Manunuzi na Kamati ya Ukaguzi ili kusimamia uwajibikaji katika utendaji kazi na matumizi ya fedha za Serikali.

44. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2022/23, Tume ya UKIMWI iliidhinishiwa jumla ya shilingi 519,603,240.00 ambapo kati ya hizo shilingi milioni 286,033,245.00 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 233,569,995 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2023, Tume imeingiziwa shilingi milioni 582,868,890.00 ambayo ni sawa na asilimia 112 ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi 386,215,890.00 sawa na asilimia 135 ni mishahara ya wafanyakazi na shilingi 196,653,000.00 sawa na asilimia 84 kwa matumizi mengineyo. Aidha, Tume imepokea fedha za Washirika wa Maendeleo shilingi milioni 140,256,500 kwa ajili ya programu za afya ya uzazi na vijana na shilingi 179,996,134 zilizopelekwa kwa asasi za kiraia kutekeleza programu ya makundi maalum.

***Utekelezaji wa Programu za Ofisi Kuu – Fungu B01***

45. **Mheshimiwa Spika** Fungu B01 linasimamia Programu tatu ambazo programu ya Usimamizi wa Mazingira na Uratibu wa Mabadiliko ya Tabianchi, Programu ya Watu wenye Ulemavu na Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

**Programu ya Usimamizi wa Mazingira na Uratibu wa Mabadiliko ya Tabianchi**

46. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imetembelea jumla ya Asasi za Kiraia 12 za Uhifadhi wa Mazingira katika Wilaya ya Kati

(2), Wilaya ya Kusini (3), Wilaya ya Magharibi A (4) na Wilaya ya Magharibi B (3) kwa lengo la kuangalia utendaji kazi wa Jumuiya hizo. Aidha, elimu ya uhifadhi na utunzaji wa mazingira imetolewa katika jumuiya za SOLIEVA (Kianga), MKODEA (Mwera) na FUPEKO (Fumba) ambapo jumla ya watu 72 walipatiwa elimu hiyo.

47. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi pia ilishiriki maonesho ya Kitaifa ya Tamasha la Biashara ya kuadhimisha miaka 59 ya Mapinduzi ya Zanzibar katika viwanja vya Maisara Unguja ambapo elimu juu ya uhifadhi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi imetolewa. Vile vile, Ofisi ilishiriki katika upandaji wa mikoko eneo la Unguja Ukuu – Uzi uliondaliwa na Jumuiya ya ZAVECO. Aidha, vipindi vitatu vya redio na kimoja cha televisheni vimerushwa hewani.

**Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Watu wenye Ulemavu**

48. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu limetoa jumla ya visaidizi 852 Unguja na Pemba, kwa upande wa Unguja jumla ya visaidizi 469 vimetolewa (wanawake 240 na wanaume 229) na kwa Pemba visaidizi 383 (wanawake 250 na wanaume 133). Ofisi imeendelea kufanya usajili na uhakiki wa taarifa za Watu wenye Ulemavu ili kupata taarifa sahihi zitakazosaidia katika kuandaa mipango mbali mbali ya Baraza. Ofisi pia imeadhimisha Siku ya Kimataifa ya Watu wenye Ulemavu tarehe 3 Disemba 2022. katika viwanja vya Gombani ya

Kale, Mkoa wa Kusini Pemba, Wilaya ya Chake chake ambapo mgeni Rasmi alikuwa ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Othman Masoud Othman.

**49.** **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imefuatilia marejesho ya fedha za mikopo zilizotolewa kwa mtu mmoja mmoja na vikundi vya ujasiriamali vya Watu wenye Ulemavu ambapo jumla ya shilingi 41,651,500.00 zimelipwa. Jumla ya Ruzuku ya shilingi 15,000,000.00 zilitolewa kwa jumuiya 6 za Watu wenye Ulemavu ambazo ni Shirikisho la Michezo ya Viziwi Zanzibar, Jumuiya ya Wasioona, Umoja wa Watu wenye Ulemavu, Jumuiya ya Malbino Zanzibar na Jumuiya ya Usalama Barabarani - Zanzibar. Lengo la fedha hizo ni kuzisaidia jumuiya hizo katika shughuli zao za kila siku. Vile vile, Ofisi imekalimisha malipo kwa vijana watatu wenye ulemavu (mwanaume mmoja na wanamke wawili) waliojiendeleza na masomo katika Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA). Aidha, vikundi 31 vya ujasiriamali vya Watu wenye Ulemavu vimetembelewa (20 Unguja na 11 Pemba). Ofisi imeratibu vikundi vya ujasiriamali 9 vilivyopata pesa ya ahuweni ya UVIKO 19 (Unguja 3 na Pemba 6) kwa lengo la kuvipatia elimu ya ujasiriamali ili kuvijengea uwezo na kuhakikisha Watu wenye Ulemavu wanachangia katika kukuza pato la taifa pamoja na kuwaongezea thamani katika bidhaa zao.

**50.** **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imefanya ziara katika skuli 11 kwa Unguja na Pemba kwa lengo la kuwalinda na kuwatetea Watu wenye Ulemavu, pamoja na kuangalia maendeleo na

changamoto zinazowakabili wanafunzi hao ili kushirikiana na wahusika katika kutafuta ufumbuzi. Aidha, mafunzo ya ukalimani wa lugha ya alama yalitolewa kwa walimu 40 (wanawake 36 na wanaume 4) wanaowafundisha wanafunzi wenye ulemavu wa uziwi na wanaoandaliwa kwenda kufundisha katika skuli ya Mjumuisho iliyopo Jendele Wilaya ya Kati Mkoa wa Kusini Unguja. Vile vile majengo mapya 22 yakiwemo ya hospitali za wilaya na skuli Unguja na Pemba yametembelewa. Lengo la ziara hizo ni kuona namna mazingira rafiki ya Watu wenye Ulemavu kama yamezingatiwa. Aidha, Ofisi iliendelea kufanya warsha kwa washiriki 89 juu ya kukinga ulemavu kupitia ajali za barabarani kwa waendesha bodaboda, bajaji, jeshi la polisi kupitia kitengo cha usalama barabarani na mabaguani.

**Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais**

51. **Mheshimiwa Spika,** sehemu hii inaelezea utekelezaji katika program za Uratibu wa Shughuli za Ofisi ya Faragha ya Makamu wa Kwanza wa Rais; Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti; Utumishi na Uendeshaji; na Uratibu wa Ofisi Pemba. Kwa kipindi cha Julai – Machi, 2023, programu hii imetekeleza yafuatayo: -

**Programu ya Uratibu wa Shughuli za Ofisi ya Faragha**

52. **Mheshimiwa Spika,** kupitia programu hii Ofisi imeendelea kuratibu shughuli za kila siku za Mheshimiwa Makamu

wa Kwanza wa Rais zikiwemo kuimarisha upatikanaji wa huduma nyumbani na Ofisini, kufuatilia utekelezaji wa ahadi anazozitoa na kero za wananchi mbali mbali wanaofika ofisini kwa Makamu na kuzitafutia ufumbuzi.

53. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Faragha imeratibu ziara mbali mbali za kikazi za ndani ya nchi za Mheshimiwa Makamu kwa lengo la kusaidia kufuatilia utekelezaji wa miradi na mipango ya Serikali. Vikao vya Mheshimiwa Makamu na Kamati Teule mbali mbali viliratibiwa na kumuwezesha kutoa maoni yake. Kamati hizo ni pamoja na Kamati ya Kuimarisha Mfumo wa Elimu Zanzibar, Kamati ya Haki Jinai, Kamati ya Tathmini ya Hali ya Kisiasa na Kamati ya Tathmini ya Utendaji wa Wizara ya Mambo ya Nje. Vile vile, mikutano ya Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais na wageni mbali mbali wakiwemo viongozi wa ndani na nje ya nchi imefanyika kwa lengo la kuimarisha mahusiano.

**Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti**

54. **Mheshimiwa Spika,** kupitia programu hii, Ofisi imekamilisha maandalizi ya Sera ya Dawa za Kulevya. Aidha, Sheria ya Watu wenye Ulemavu nam. 8/2022 imekamilika na kuanza kutumika. Sheria hii imeweka masharti yanayohusiana na Watu wenye Ulemavu yenye lengo la kuimarisha mfumo, miundo na taratibu katika kusimamia masuala ya Watu wenye Ulemavu ili kuhakikisha

Watu wenye Ulemavu wanafaidika kikamilifu na haki za binaadamu, huduma, na fursa mbali mbali na kuimarisha ustawi wa maisha yao na hatimae kuwa na jamii jumuishi. Vile vile, Kanuni za sheria hii zimeratibiwa na zinafanyiwa kazi katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Aidha, Muongozo wa Ugawaji wa visaidizi na Muongozo wa Mfuko wa Maendeleo ya Watu wenye Ulemavu inatayarishwa.

55. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imekamilisha maandalizi ya Mpango Mkakati na hatua za utekelezaji zinaendelea. Aidha, Ofisi imeratibu mapitio ya vifungu katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira namba 3/2015 ili iweze kukidhi haja ya wakati huu ya usimamizi wa masuala ya bioteknolojia ya kisasa pamoja na ushiriki wa Zanzibar katika biashara ya kaboni. Kanuni mbili za Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya zimeratibiwa. Ofisi imeshiriki katika utafiti wa Hali ya UKIMWI nchini unaofanyika Tanzania nzima ili kubaini mwenendo wa jitihada za kudhibiti ugonjwa huu na kuimarisha mapambano. Aidha, programu ya Kuirithisha Zanzibar ya Kijani imeandaliwa na kuanza utekelezaji wake.

**Programu Ndogo ya Utumishi na Uendeshaji**

56. **Mheshimiwa Spika,** kupitia programu hii, miundombinu ya jengo la Ofisi inaendelea kuimarishwa zaidi kwa uwekaji wa lifti ambapo hivi sasa mchakato wake upo katika hatua ya vikao vya Bodi ya Zabuni. Aidha, matengenezo madogo madogo ya jengo la ofisi yanaendelea kufanyika

kwa dhamira ya kuweka mazingira ya Ofisi katika hali nzuri. Vile vile, huduma mbali mbali za Ofisi zikiwemo usafi, ununuzi wa mafuta, vifaa vya kuandikia, thamani, matengenezo ya vyombo vya usafiri zimeendelea kutolewa ili kuiwezesha ofisi kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

57. **Mheshimiwa Spika,** mazingira ya utendaji kazi kwa watumishi yameendelea kuimarishwa kwa kuwapatia stahiki za likizo na malipo baada ya saa za kazi. Aidha, ofisi imelipa nyongeza za mishahara iliyotokana na kupandishwa kwa mishahara kwa watumishi wote. Aidha, watumishi watano wameendelea kulipiwa ada ya mafunzo ya muda mrefu katika Manunuzi na Uondoaji Mali za Umma, Rasilimali watu, Sheria, Usimamizi wa Miradi ya kimaendeleo, watumishi watano wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika fani ya udereva wa Viongozi na fani ya Uongozi na watumishi 50 wamepatiwa mafunzo ya ndani "inservice training" katika nyanja tofauti zikiwemo maadili ya utumishi wa umma, usalama na afya kazini, TEHAMA, asset register, kumbukumbu, uhazili na ofisi mtandao.

58. **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza agizo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar la kuzitaka Taasisi zote kutumia mifumo ya Ofisi mtandao na manunuzi mtandao yaani "e-office na e-procurement tayari Ofisi imeshaanza na inaendelea kutumia mifumo hiyo katika utekelezaji wa shughuli zake za kila siku.

**Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba**

**59.** **Mheshimiwa Spika,** kupitia programu hii Ofisi imeendelea kuratibu shughuli zote za Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa upande wa Pemba. Shughuli hizo ni pamoja na kufanya ziara katika maeneo mbali mbali yaliyopo Pemba ili kuangalia athari ya mabadiliko ya tabia nchi na kukagua athari za uchimbaji wa matofali pamoja na kifusi katika sehemu ya Uwandani na Kangagani. Aidha, Ofisi imefanya ziara za kukutana na va vikundi vya Watu wenye Ulemavu, Jumuiya zinazoshughulikia masula ya UKIMWI na waraibu wanaotumia dawa za kulevya kwa nyakati tofauti.

**60.** **Mheshimiwa Spika,** uratibu wa shughuli za miradi umefanyika, ukiwemo mradi wa Msingini unaoimarisha mfumo wa maji machafu na mradi wa Sipwese wa kujenga ukuta na kivuko. Ofisi iliratibu maadhimisho ya Siku ya UKIMWI Duniani, ilishiriki maonesho ya Siku ya Chakula Duniani pamoja na kuratibu maadhimisho ya Siku ya Watu Wenye Ulemavu. Ziara za Viongozi Wakuu wa Kitaifa na wageni wengine mbali mbali ziliratibiwa ikiwemo ziara zilizolenga kuangalia athari za kimazingira.

**61.** **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Idara ya Watu wenye ulemavu Ofisi imesimamia ukamilishaji wa ujenzi wa sehemu ya kufanyia kazi kwa Kikundi cha Watu wenye Ulemavu Shehia ya Majenzi Wilaya ya Micheweni kikundi cha NGUVU MOJA USHONI. Ofisi imesimamia

ugawaji wa vyandarua vilivyotolewa msaada na Korea Cultural Foundation and Malaria Education Foundation for Zanzibar. Vile vile, imesimamia ununuzi wa tenki la maji, mpira, mchikichi na kukifanyia matengenezo Kisima cha mzazi mwenye watoto sita wenye ulemavu katika Wilaya ya Wete Shehia ya Kinyasini.

**62.** **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imesimamia marekebisho ya kisima, kujenga mnara, ununuzi wa tenki moja, mchikichi na vifaa vya umwagiliaji katika kikundi cha Mikakati kilichopo Vitongoji Wilaya ya Chake Chake. Vile vile, Ofisi imesimamia ujenzi wa minara miwili, sehemu ya kulia pamoja na jiko katika makaazi ya Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar huko Micheweni Pemba.

**63.** **Mheshimiwa Spika,** katika uimarishaji utendaji kazi Ofisi imefanya ununuzi wa honda moja, kompyuta mbili, printa, skana, sare za watumishi, mashine ya kuingia na kutoka kazini (biometric), kulipa stahiki za likizo kwa watumishi, ununuzi wa umeme, vifaa vya kuandikia pamoja na kufanya matengenezo ya Ofisi.

**64.** **Mheshimiwa Spika,** Programu za Fungu B01 ziliidhinishiwa jumla ya shilingi 5,055,618,768.00. Kati ya fedha hizo jumla ya shilingi 1,846,800,000.00 ziliidhinishwa kwa ajili ya mishahara, na shilingi 3,208,818,768.00 zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2023, jumla ya fedha zilizopatikana ni shilingi 3,146,308,845.00 sawa na asilimia 62 zinazojumuisha shilingi

2,211,847,645.00 sawa na asilimia 120 za mishahara na shilingi 934,461,200.00 sawa na asilimia 29 kwa matumizi mengineyo. *Kiambatanisho nam 1 kinahusika.*

## F. MWELEKEO WA BAJETI KWA MAFUNGU YA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA MWAKA 2023/2024

**65. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ina Mafungu ya kibajeti manne ambayo ni:- B01 la Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Ofisi Kuu; B04 - Fungu la Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira (ZEMA), Fungu C04 la Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya; na Fungu C05 la Tume ya UKIMWI. Maelezo yafuatayo yanatoa mwelekeo wa bajeti kwa Taasisi zinazojitegemea.

***Mwelekeo wa Bajeti Kwa Taasisi za Ofisi ya Makamu Wa Kwanza Wa Rais***

***Fungu B04 Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira***

**66. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inakusanya mapato kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira. Kwa mwaka 2023/2024, Ofisi inakadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 574,100,000.00 ambazo zinatokana na ada ya uhifadhi na ada ya ukaguzi wa mazingira ili kuchangia mapato ya Serikali.

**67. Mheshimiwa Spika,** Fungu B04 linasimamia Programu Kuu mbili ambazo ni Programu ya Usimamizi wa Mazingira na Programu ya Utumishi na Uendeshaji. Kwa mwaka 2023/2024 Ofisi kupitia programu hizi imejipangia kuendeleza kusimamia utekelezaji wa sheria, kanuni, viwango na miongozo ya kimazingira; kuhakikisha kuwa miradi yote inafanyiwa tathmini za kimazingira ili kuifanya miradi hiyo kuwa endelevu bila ya kusababisha uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Ofisi pia imedhamiria kuendelea na kufanya ufuatiliaji kwenye miradi na maeneo mbali mbali utakaosaidia kupatikana kwa usimamizi endelevu wa mazingira.

**68. Mheshimiwa Spika,** ili kuliwezesha Fungu B04 liweze kutekeleza majukumu yake naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha shilingi 1,574,000,000.00. Mchanganuo wa fedha hizi unapatikana katika *kiambatanisho nam 2 kinahusika.*

***Fungu C04 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya***

**69. Mheshimiwa Spika,** Fungu C04 linasimamia Programu Kuu mbili ambazo ni Programu ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya na Programu ya Utawala na Rasilimali watu. Kwa mwaka 2023/2024 Ofisi kupitia programu hizi imejipangia kudhibiti na kuendeleza mapambano juu ya usafirishaji, usambazaji, na utumiaji wa dawa za kulevya. Kituo cha Huduma za Pamoja cha Uendeshaji wa Kesi za dawa za

kulevya na Programu za Upataji Nafuu zitaendeshwa pamoja na kuendeleza ujenzi na uendeshaji wa Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia Kidimni. Mamlaka itafanya zoezi la kuteketeza kisheria dawa za kulevya zilizohifadhiwa na kufuatilia na kutaifisha mali zinazotokana na uhalifu wa dawa za kulevya.

70. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa Sheria namba 8/2021 inaipa Mamlaka uwezo wa upelelezi, Ofisi itachukua hatua za kuwajengea uwezo watendaji wake kwa kushirikiana na wadau mbali mbali. Aidha, Mamlaka itatayarisha na kuweka miongozo (manuals) itakayotumika katika utekelezaji wa majukumu yake. Jamii itajengewa uelewa juu ya sheria namba 8/2021 ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, athari za matumizi ya dawa za kulevya na kuhusu kuimarisha kinga ya msingi dhidi ya matumizi ya dawa hizo. Vile vile, Ofisi itaimarisha mahusiano na taasisi nyengine za Kitaifa, Kikanda na Kimataifa kwa kushiriki vikao mbali mbali vya kupambana na dawa za kulevya na kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi watumishi wa Mamlaka ili kwenda sambamba na kasi ya mapambano dhidi ya dawa za kulevya na uhalifu unaofanana nao.

71. **Mheshimiwa Spika,** ili kuliwezesha Fungu C04 liweze kutekeleza majukumu yake naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 3,247,684,987.00 zikiwemo shilingi 1,747,684,987.00 kwa kazi za kawaida na shilingi 1,500,000,000.00 kwa kazi za maendeleo. Mchanganuo wa fedha hizi unapatikana katika *kiambatanisho nam. 2*.

*Fungu C05 Tume ya UKIMWI*

72. **Mheshimiwa Spika,** Fungu C05 linasimamia Programu Kuu mbili ambazo ni Programu ya Kuratibu Muitiko wa Taifa wa UKIMWI na Programu ya Utumishi na Uendeshaji. Kwa mwaka 2023/2024. Bajeti hii imezingatia maelekezo ya Serikali ya kuimarisha huduma za afya ikiwemo VVU na UKIMWI na kwenda sambamba na vipaumbele vya Serikali vya kuimarisha miundo mbinu ya bandari, barabara na viwanja vya ndege. Mwelekeo wa Bajeti hii umetokana na Mkakati wa Tume ambao unalenga kuifanya Tume kuwa ni taasisi yenye ufanisi katika kutimiza majukumu yake ya msingi.

73. **Mheshimiwa Spika,** Tume ya UKIMWI itaendelea kusimamia muitiko wa taifa dhidi ya UKIMWI kwa kuweka Miongozo ya Kitaifa na mikakati ya kudhibiti maambukizo mapya ya VVU katika jamii na katika utekelezaji wa miradi kwa kutilia mkazo makundi ya vijana, wanawake na makundi maalum ambao wanaambukizwa zaidi na maeneo ambayo yanapitiwa na miradi mikubwa. Ofisi itauweka katika lugha nyepesi Mkakati wa Nne wa Taifa wa UKIMWI ili iwe rahisi kufahamika na wadau wote. Aidha, Ofisi itaandaa Mkakati wa Mawasiliano na Mabadiliko ya tabia kwa vijana na itaifanyia mapitio Sheria ya Kukinga na Kusimamia Masuala ya UKIMWI ili iweze kwenda sambamba na hali ya sasa na mabadiliko ya kisayansi ya kinga na tiba ya VVU na UKIMWI na kuufikisha muongozo wa utayarishaji wa program za VVU katika miradi kwa sekta husika.

**74.** **Mheshimiwa Spika,** Tume ya UKIMWI itaendelea kuimarisha uwezo wa sekta mbali mbali wa kuzingatia masuala ya VVU na UKIMWI katika utekelezaji wa kazi za msingi na miradi ya maendeleo kwa kuweka miongozo, kufanya kazi na taasisi zinazosimamia miradi hiyo na kuziratibu taasisi zote. Aidha, itafanya tafiti kila mwaka ili kupata taarifa sahihi zitakazosaidia kuandaa mipango ya VVU na UKIMWI inayoakisi mahitaji ya makundi mbali mbali kwa kuzishirikisha sekta zote. Vile vile, itaimarisha uwezo wa wafanyakazi wa Tume ili kuongeza ufanisi wa kazi kwa kuendelea kugharamia mafunzo yao ya muda mrefu na kuwapatia watendaji wote mafunzo msasa ili kuongeza ujuzi wa kutenda kazi zao.

**75.** **Mheshimiwa Spika,** ili kuliwezesha Fungu C05 liweze kutekeleza majukumu yake naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 1,210,233,000 za Matumizi ya Kawaida. Mchanganuo wa fedha hizi unapatikana katika *kiambatanisho nam. 2.*

**Mwelekeo wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais**

**76.** **Mheshimiwa Spika,** Vipaumbele vya Ofisi kwa Mwaka 2023-2024 ni hivi vifuatavyo:-

i. Kutekeleza Programu ya Kuirithisha Zanzibar ya Kijani (Zanzibar Green Legacy Programme) na kuendelea kushughulikia athari za mabadiliko ya tabianchi.

ii. Kuimarisha utekelezaji wa Sheria ya Watu wenye Ulemavu nam. 8/2022;

iii. Kuendelea kutekeleza Sheria ya Dawa za Kulevya nam. 8/2021 inayoimarisha mapambano dhidi ya dawa za kulevya ili hatimaye tuweze kuinusuru jamii yetu na athari zinazosababishwa na biashara na matumizi ya dawa za kulevya;
iv. Kuendelea kupiga vita UKIMWI kwa kuendesha programu za kukuza mwitiko wa jamii ili hatimaye tuweze kuuondoa UKIMWI katika orodha ya magonjwa hatarishi;
v. Kuendelea kuelimisha jamii kuhusu uhifadhi wa mazingira, kujikinga na maambukizi mapya ya UKIMWI na kuepuka kusambaza UKIMWI kwa makundi rika; kushajihisha jamii kuwajali, kuwahudumia na kuwaendeleza Watu wenye Ulemavu na kuimarisha vita dhidi ya dawa za kulevya kwa kufanya kampeni mbali mbali katika ngazi ya jamii; na
vi. Kuimarisha uratibu wa masuala yanayosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

**Mwelekeo wa Matumizi kwa Programu za Ofisi Kuu – Fungu B01**

**77. Mheshimiwa Spika,** fungu hili lina Programu Kuu tatu zinazosimamiwa na Katibu Mkuu, ambazo ni:-

i. Programu ya Usimamizi wa Mazingira na Uratibu wa Mabadiliko ya Tabianchi;
ii. Programu ya Watu wenye Ulemavu; na
iii. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

**Programu ya Usimamizi wa Mazingira na Uratibu wa Mabadiliko ya Tabianchi**

78. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Ofisi kupitia programu hii imejipangia kupitia Sera ya Mazingira ya mwaka 2013, kupitia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2015, kutayarisha Mpango wa Kitaifa wa Mazingira, kufanya tafiti ya kuyatambua maeneo yaliyoathirika na mabadiliko ya tabianchi Pemba, kuongeza uelewa kwa jamii juu ya uhifadhi wa mazingira kupitia mikutano, vipindi vya TV na redio, kuadhimisha siku ya Mazingira Duniani, kushiriki maonesho ya Kitaifa pamoja na kuratibu shughuli za uendeshaji wa ofisi.

79. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa shughuli za maendeleo, programu imejipangia kutekeleza mradi wa Kuimarisha Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa jamii za pwani ya Zanzibar kwa kujenga uwezo wa wakulima wadogo kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa njia za vitendo na ubunifu ambazo zitakuwa na matokeo yenye tija. Vile vile, kuendeleza maeneo yaliyoharibika kimazingira kutokana na mabadiliko ya tabianchi ambayo ni Msuka, Kisiwa Panza na Sipwese Pemba. Aidha, kushajihisha uhifadhi wa Mazingira kupitia Programu ya Kuirithisha Zanzibar ya Kijani kwa upandaji miti katika Wilaya zote ili kuimarisha na kuhuisha uoto wa asili pamoja na uhifadhi wa vyanzo vya maji. Kufanya tathmini ya kina kwa maeneo mbali mbali Unguja na Pemba ambayo yameathirika na mabadiliko ya tabianchi (Vulnerability

Assessment) ili kupata taarifa sahihi zitazopelekea kuweka mkakati madhubuti wa kukabiliana na athari hizo na uimarishaji wa jamii na usimamizi endelevu wa ikolojia na shughuli za kujipatia kipato kwa wavuvi wadogo katika Eneo la Hifadhi ya Mkondo wa Pemba.

**Programu Kuu ya Watu wenye Ulemavu**

80. **Mheshimiwa Spika,** mwelekeo wa Bajeti ya Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu ni Uwezeshaji wa Watu wenye Ulemavu, lengo letu ni kuiwezesha jamii ya Watu wenye Ulemavu ili waweze kujitegemea na kuendesha maisha yao binafsi. Aidha, ujumuishwaji wa masuala ya Watu wenye Ulemavu katika programu mbali mbali za kitaifa na kimataifa limepewa kipaumbele na kuhakikisha Watu wenye Ulemavu wanafikia huduma kama watu wasio na ulemavu. Katika kipindi hiki, Baraza limetenga fedha za ruzuku kwa ajili ya kuwawezesha Watu wenye Ulemavu kupitia Mfuko wa maendeleo ya Watu wenye Ulemavu Zanzibar. Nachukua fursa hii kuishukuru Serikali kwa kutupatia ruzuku hii.

81. **Mheshimiwa Spika;** Baraza litaendelea kuongeza uelewa kwa jamii juu ya masuala ya Watu wenye Ulemavu, hususani, kupinga unyanyapaa, udhalilishaji na kuondosha fikra potofu juu ya watu wenye ulemavu kupitia vipindi vya Radio na TV pamoja na mikutano ya jamii.

**Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais**

82. **Mheshimiwa Spika,** katika sehemu hii tutaelezea mipango yetu katika programu zinazohusu uratibu wa shughuli za Ofisi ya Faragha, Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti, Usimamizi wa Rasilimali-watu na Uendeshaji wa Ofisi, na Uratibu wa Shughuli za Ofisi Pemba. Kwa mwaka 2023/2024 programu hii imepanga kutekeleza yafuatayo:-

**Programu ya Uratibu wa Shughuli za Ofisi ya Faragha**

83. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamia masuala yote yanayohusiana na utoaji wa huduma kwa ofisi na makaazi ya Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais. Kwa mwaka 2023/2024, programu hii imepanga kuhakikisha huduma zinaendelea kutolewa kwa Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais. Ofisi ya Faragha itaendelea kuhakikisha kuwa Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais anaendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kusimamia vyema shughuli alizokasimiwa ikiwemo kusimamia utekelezaji wa sera zinazoongoza Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

84. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024, Ofisi kupitia program ya uratibu wa shughuli za Makamu wa Kwanza wa Rais imepanga kufanya yafuatayo:-

i. Kuratibu ziara za ndani na nje za Makamu wa Kwanza wa Rais;

ii. Kuratibu ufuatiliaji wa ahadi na maagizo ya Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais;
iii. Kuratibu Vikao vya Mabalozi na Wageni kwa ajili ya kuimarisha mahusiano na mashirikiano; na
iv. Kufanya matengenezo madogo madogo ya makaazi ya Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais Unguja na Pemba.

**Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti**

**85. Mheshimiwa Spika,** ofisi itaendelea kuratibu maandalizi ya nyaraka mbali mbali za ofisi ikiwemo Sera ya Mazingira na Sera ya UKIMWI, itajenga uelewa wa wananchi kuhusu majukumu ya Ofisi na itaratibu utekelezaji wa Programu ya Kuirithisha Zanzibar ya Kijani. Katika kipindi hiki Ofisi itaendelea na uratibu wa marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira 3/2015, Sheria ya uanzishwaji wa Tume ya UKIMWI 3/2002, na Sheria ya Kusimamia na Kukinga masuala ya UKIMWI 18/2013. Ofisi pia itaendelea kuratibu tafiti na kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa shughuli za kawaida na miradi ya maendeleo inayosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

**Programu Ndogo ya Utumishi na Uendeshaji**

**86. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais itaendelea kuimarisha miundombinu ya jengo kwa kuendelea na hatua ya uwekaji

wa lifti hasa ikiwa utekelezaji wake hautaweza kukamilika ndani ya robo ya mwisho ya bajeti ya 2022/2023, kurekebisha mfumo wa umeme ndani ya jengo, ujenzi wa vyumba vya nje vya ofisi, kuimarisha mfumo wa Kamera za CCTV, kuvifanyia matengenezo vyombo vya usafiri, kufanya matengenezo madogo madogo ya ofisi.

**87.** **Mheshimiwa Spika,** Ofisi itaendelea kusimamia shughuli za kiutawala na kuhakikisha kuwa mazingira ya utendaji kazi yanaendelea kuimarika kwa upatikanaji wa huduma mbali mbali zikiwemo usafi, ununuzi wa vifaa vya kuandikia, mafuta pamoja na samani. Vile vile, ofisi itahakikisha kuwa stahiki za watumishi zinaendelea kupatikana ikiwa ni pamoja na kuwaendeleza watumishi kwa kuratibu mafunzo ya muda mrefu na mfupi, mafunzo ya ndani katika nyanja za rasilimali watu, uongozi, habari, tehama, sheria, na mafunzo kwa watumishi wapya.

**88.** **Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa matakwa ya Sheria ya Utumishi wa Umma katika Ofisi ya Makamu wa kwanza wa Rais utaendelea kwa kuzingatia maelekezo, matoleo na miongozo mbali mbali kwa dhamira ya kuongeza kasi zaidi ya uajibikaji na kuimarisha zaidi utendaji kazi.

**Programu Ndogo ya Uratibu Shughuli za Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba**

**89.** **Mheshimiwa Spika,** Ofisi Kuu Pemba kwa mwaka wa Fedha 2023-2024 itaendelea kuratibu shughuli

zinazofanywa na Idara zilizoko chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kuratibu ziara za Viongozi Wakuu wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na wageni watakaofika Kisiwani Pemba kwa shughuli mbalimbali.

**90.** **Mheshimiwa Spika,** vile vile, Ofisi itaendelea kusimamia miradi inayotekelezwa Kisiwani Pemba, kusimamia matengenezo ya Makaazi ya Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais huko Micheweni. Katika uimarishaji utendaji kazi Ofisi itaendelea kuwapatia watumishi wake mafunzo ya muda mrefu na mfupi, kuwapatia Watumishi stahiki zao pamoja na ununuzi wa vifaa vya utendaji kazi.

**91.** **Mheshimiwa Spika,** ili kuliwezesha Fungu B01 liweze kutekeleza majukumu yake naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 10,746,511,388.00 zikiwemo shilingi 5,595,700,000.00 kwa matumizi ya kawaida na shilingi 4,951,011,388.00 za maendeleo. Mchanganuo wa fedha hizi unapatikana katika *kiambatanisho nam. 2.*

## G. SHUKURANI

**92.** **Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia, nachukua fursa hii adhimu, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kuwasilisha hotuba hii mbele yenu. Nawaomba radhi kwa mapungufu yoyote yaliyojitokeza. Naomba nitambue mashirikiano makubwa ninayoyapata kutoka kwa Watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, wakiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. Omar Dadi Shajak na

Wakuu wa Taasisi na Idara zote zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa kwanza wa Rais. Naomba pia niwashukuru sana wahusika wote waliochangia kufanikisha utendaji wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Michango, maelekezo na ushauri wao umesaidia sana, kuongeza kasi ya utendaji kwa kuleta mafanikio ya utekelezaji wa majukumu yetu. Miongoni mwao ni:-

i. Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

ii. Ofisi ya Waziri Mkuu,

iii. Baraza la Taifa la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC),

iv. UNDP, UNEP, GEF, GCF, UNODC, UK- Border Force, British Kingdom, UNFPA, UNICEF, Global Fund, PEPFAR, UNAIDS, n.k.

v. Nazishukuru taasisi zote zisizo za kiserikali zinazofanya kazi na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na ninawashukuru sana Viongozi wa Dini katika kutusaidia kujenga imani za waumini katika kupambana na dawa za kulevya, maambukizo ya ukimwi, uhifadhi wa mazingira na kuwajali watu wenye ulemavu; na

vi. Kwa namna ya kipekee navishukuru sana vyombo vya habari vya Serikali na binafsi kwa kuiunganisha vizuri sana Ofisi yetu na jamii. Mchango wao unasaidia sana katika kurahisisha utekelezaji wa majukumu yetu ya kila siku.

## H. HITIMISHO

93. **Mheshimiwa Spika,** naomba nimalizie kwa kusisitiza kuwa, utekelezaji wa Programu ya Kuirithisha Zanzibar ya Kijani ni mtambuka, inatuhusu kila mtu, hivyo nasisitiza kuwa program hii inahitaji mashirikiano yetu sote katika ngazi mbali mbali na kupitia jitihada za washirika mbali mbali. Kwa mantiki hiyo, tunapaswa kuzitafuta na kuzitumia fursa zote zilizopo ili kutekeleza shughuli zitakazopelekea kufikiwa kwa malengo yetu ya Kuirithisha Zanzibar ya Kijani kwa faida ya kizazi cha sasa na cha baadae. Naomba nitoe wito kwa kila seka katika eneo lake la kiutendaji, ione umuhimu wa utekelezaji wa programu hii. Aidha, niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuchukua jitihada za makusudi kuhakikisha kuwa majimbo yetu yanashindana katika kuimarisha uoto wa asili, kupanda miti, kuitunza na kutekeleza mabadiliko katika jamii yetu kupenda miti. Wizara inayohusika na Nishati itajitahidi kutafuta mbinu mbadala za nishati ya kupikia na kuwapa wananchi wetu unafuu katika upatikanaji na gharama zake. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inatambua kuwa Vikosi vyetu vya Ulinzi na Usalama zikiwemo Idara Maalum za SMZ vinaweza kuwa mfano wa kuigwa katika utekelezaji wa Programu hii ya Kuirithisha Zanzibar ya Kijani. Haya shime twende sote tuimarishe mazingira na vile vile kuyapendezesha. Tujifunze na tutumie mbinu zilizofanikiwa katika nchi za wenzetu kwa kujenga barabara zilizopambwa na miti na maua, na tuzipambe Ofisi na mazingira yake kwa miti na bustani kila inapowezekana.

94. **Mheshimiwa Spika,** naomba pia niwaombe wana jamii katika maeneo yetu tunayoishi kila mmoja kwa nafasi yake, ashiriki kikamilifu kubadilika na kupanda miti aina kwa aina itakayotupatia matunda, lakini pia itakayotuwezesha kujenga uchumi kupitia uzalishaji na uuzaji wa miti kupitia miradi mipya ya kisasa ya biashara ya kaboni. Hali hii itasaidia kuweka uwiano uzuri wa matumizi na uzalishaji wetu wa bidhaa za misitu.

95. **Mheshimiwa Spika,** naomba pia nitumie fursa hii kuziomba sekta zote zilizoguswa katika Sheria ya Watu wenye Ulemavu inayotutaka sote kuzingatia masuala ya Watu wenye Ulemavu katika mipango na utekelezaji wa mipango yetu ili kulinda haki zao kama zilivyobainishwa katika Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984, Mikataba ya Kikanda na Kimataifa na ni katika kutimiza wajibu wetu katika kujenga jamii bora inayoheshimu haki za kila mtu.

96. **Mheshimiwa Spika,** naomba kusisitiza kuwa UKIMWI bado upo, maambukizi bado ni makubwa baina ya makundi maalum ambayo uwezekano wake wa kuchanganyika na makundi mengine ni mkubwa, hali ambayo inaweza kupelekea kuturudisha tulikotoka. Namuomba Mwenyeezi Mungu atuwezeshe kumaliza UKIMWI kama janga la kitaifa na kimataifa haraka iwezekanavyo kwa kuhakikisha sote tunajikinga na maambukizo mapya, tunatoa huduma stahiki kwa walioathirika, tunaondoa unyanyapaa na tunazingatia usawa. Kwa kumalizia naomba tuendeleze mapambano dhidi ya uingizaji, usambazi na matumizi

ya dawa za kulevya na tutoe huduma stahiki kwa vijana na ndugu zetu ambao tayari wameathirika na matumizi ya dawa za kulevya. Aidha, tuwalinde watoto wetu na matumizi ya dawa hizo pamoja na janga hili lililoingia kwa kasi la udhalilishaji na mapenzi ya jinsia moja. Sote tushirikiane kujenga umma bora wenye maadili na silka za kizanzibari na kiafrika.

97. **Mheshimiwa Spika,** ninawashukuru wananchi wenzangu wa Jimbo la Wete kwa mashirikiano ya pamoja ya kulileteа maendeleo Jimbo letu. Aidha, ninaishukuru sana familia yangu kwa kuweza kunivumilia na kuniunga mkono katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku ya kiuongozi katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

98. **Mheshimiwa Spika,** naomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu waichangie hotuba hii, watushauri ipasavyo na hatimaye waiidhinishie Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais matumizi ya shilingi 16,778,429,375.00 ili kutekeleza kazi za kawaida na kazi za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2023/2024, kwa mchanganuo uliotolewa. Aidha, Mheshimiwa Spika, naliomba Baraza lako tukufu liikubalie Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ichangie kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali jumla ya shilingi 574,100,000.00 zitakazokusanywa kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira.

**Mchanganuo wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

| Taasisi/Idara | Kiasi (Shilingi) |
|---|---|
| Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya | 3,247,684,987 |
| Tume ya UKIMWI | 1,210,233,100 |
| Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira (ZEMA) | 1,574,000,000 |
| Ofisi ya Faragha | 1,199,684,700 |
| Idara ya Utumishi na Uendeshaji | 1,405,998,760 |
| Idara ya Mipango, Sera na Utafiti | 340,415,720 |
| Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu | 1,186,161,320 |
| Idara ya Mazingira | 5,591,965,348 |
| Ofisi Kuu Pemba | 1,022,285,540 |
| **JUMLA KUU** | **16,778,429,375** |

**99.** **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

……………………………………………

**HARUSI SAID SULEIMAN,**
**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS ZANZIBAR**

# Kiambatanisho nam. 1(a): Muhtasari wa Upatikanaji wa Fedha Julai - Machi 2022/2023 (000)

**Kiambatanisho Nam. 1 (a) - Muhtasari wa Upatikanaji wa Fedha Julai 2022 - Machi 2023 (000)**

| Fungu/Idara | Jumla ya Fedha Zilizopangwa Kwa Miezi 9 | Mishahara na Maposho | Matumizi Mengineyo | Jumla ya Fedha Zilizopatikana kwa Miezi 9 | % | Mishahara Iliyopatikana | % | Matumizi Mengineyo Yaliyopatikana | % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idara ya Uendeshaji na Utumishi | 1,543,689 | 559,436 | 984,253 | 826,827 | **54%** | 498,659 | **89%** | 328,168 | **33%** |
| Idara ya Mipango, Sera naUtafiti | 349,535 | 97,525 | 252,010 | 157,829 | **45%** | 114,519 | **117%** | 43,310 | **17%** |
| Idara ya Watu Wenye Ulemavu | 877,384 | 286,710 | 590,674 | 522,681 | **60%** | 400,003 | **140%** | 122,679 | **21%** |
| Ofisi ya Faragha | 1,093,065 | 345,325 | 747,740 | 700,743 | **64%** | 467,250 | **101%** | 233,493 | **31%** |
| Ofisi Kuu Pemba | 893,755 | 329,388 | 564,367 | 574,865 | **64%** | 414,996 | **126%** | 159,869 | **28%** |
| Mamlaka ya Usimamizi wa | 1,149,529 | 649,819 | 499,710 | 936,496 | **81%** | 762,290 | **117%** | 174,207 | **35%** |

| Fungu/Idara | Jumla ya Fedha Zilizopangwa Kwa Miezi 9 | Mishahara na Maposho | Matumizi Mengineyo | Jumla ya Fedha Zilizopatikana kwa Miezi 9 | % | Mishahara Iliyopatikana | % | Matumizi Mengineyo Yaliyopatikana | % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mazingira (ZEMA) | | | | | | | | | |
| Idara ya Mazingira | 434,301 | 228,415 | 205,886 | 363,363 | **84%** | 316,421 | **139%** | 46,942 | **23%** |
| Tume ya UKIMWI | 519,603 | 286,033 | 233,570 | 582,869 | **112%** | 386,216 | **135%** | 196,653 | **84%** |
| Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya | 964,499 | 265,125 | 699,374 | 804,945 | **83%** | 499,273 | **188%** | 305,672 | **44%** |
| **JUMLA KUU** | **7,689,249** | **3,047,777** | **4 ,641,472** | **5,470,619** | **71%** | **3,859,626** | **127%** | **1,610,993** | **35%** |
| | | | | | | | | | |
| Jumla B01 +F | 5,055,618 | 1,846,800 | 3,208,819 | 3,146,309 | **62%** | 2,211,848 | **120%** | 934,461 | **29%** |
| Jumla Mazingira | 1,583,830 | 878,234 | 705,596 | 1,299,859 | **82%** | 1,078,711 | **123%** | 221,148 | **31%** |
| Jumla Head Office | 3,880,044 | 1,331,675 | 2,548,370 | 2,260,264 | **58%** | 1,495,424 | **112%** | 764,841 | **30%** |

**Kiambatanisho Nam. 1 (b) - Muhtasari wa Upatikanaji wa Fedha Julai 2022 - Machi 2023 Ikilinganishwa na Makadirio ya Mwaka**

| Fungu/Idara | Jumla ya Fedha Zilizopangwa kwa Mwaka | Mishahara na Maposho | Matumizi Mengineyo | Jumla ya Fedha Zilizopatikana kwa Miezi 9 | % | Mishahara Iliyopatikana | % | Matumizi Mengineyo Yaliyopatikana | % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idara ya Uendeshaji na Utumishi | 1,874,733 | 745,915 | 1,128,818 | 826,828 | **44%** | 498,659 | **67%** | 328,168 | **29%** |
| Idara ya Mipango,Sera naUtafiti | 358,034 | 130,034 | 228,000 | 157,829 | **44%** | 114,519 | **88%** | 43,310 | **19%** |
| Idara ya Watu Wenye Ulemavu | 1,070,280 | 382,280 | 688,000 | 522,681 | **49%** | 400,003 | **105%** | 122,679 | **18%** |
| Ofisi ya faragha | 1,343,174 | 460,434 | 882,740 | 700,743 | **52%** | 467,250 | **101%** | 233,493 | **26%** |
| Ofisi Kuu Pemba | 1,144,914 | 439,184 | 705,730 | 574,865 | **50%** | 414,996 | **94%** | 159,869 | **23%** |
| Mamlaka ya Usimamizi | 1,430,710 | 866,400 | 564,310 | 936,496 | **65%** | 762,290 | **88%** | 174,207 | **31%** |

| Fungu/Idara | Jumla ya Fedha Zilizopangwa kwa Mwaka | Mishahara na Maposho | Matumizi Mengineyo | Jumla ya Fedha Zilizopatikana kwa Miezi 9 | % | Mishahara Iliyopatikana | % | Matumizi Mengineyo Yaliyopatikana | % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| wa Mazingira (ZEMA) | | | | | | | | | |
| Idara ya Mazingira | 640,765 | 304,553 | 336,212 | 363,363 | **57%** | 316,421 | **104%** | 46,942 | **14%** |
| Tume ya UKIMWI | 1,288,910 | 649,030 | 639,880 | 735,343 | **57%** | 489,986 | **75%** | 245,357 | **38%** |
| Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya | 1,293,780 | 353,500 | 940,280 | 804,945 | **62%** | 499,273 | **141%** | 305,672 | **33%** |
| JUMLA KUU | 10,445,300 | 4,331,330 | 6,113,970 | 5,623,093 | **54%** | 3,963,396 | **92%** | 1,659,697 | **27%** |
| Jumla B01 | 6,431,900 | 2,462,400 | 3,969,500 | 3,146,309 | **49%** | 2,211,848 | **90%** | 934,461 | **24%** |
| Jumla Mazingira | 2,071,475 | 1,170,953 | 900,522 | 1,299,859 | **63%** | 1,078,711 | **92%** | 221,148 | **25%** |
| Jumla Ofisi Kuu | 4,720,854 | 1,775,566 | 2,945,288 | 2,260,264 | **48%** | 1,495,424 | **84%** | 764,841 | **26%** |

**Kiambatanisho nam. 2: Muelekeo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 (000)**

| Programu | Kazi za Kawaida | | | | Kazi za Maendeleo | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Jumla** | **Mishahara** | **Matumizi Mengineyo** | **SMZ** | **Wahisani** | **Jumla Maendeleo** | **Jumla Kuu** |
| Programu Kuu ya Usimamizi wa Mazingira | | | | | | | |
| **Idara ya Mazingira** | 640,954 | 422,174 | 218,780 | 3,500,000 | 1,451,011 | 4,951,011 | 5,591,965 |
| Programu Kuu ya Watu Wenye Ulemavu/Mahitaji Maalum. | | | | | | | |
| Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu | 986,161 | 538,471 | 447,690 | - | - | - | 986,161 |
| Ruzuku | | | 200,000 | | | | 200,000 |
| **Jumla Programu ya WWU** | **1,186,161** | **538,471** | **647,690** | | | | **1,186,161** |
| Progamu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais | | | | | | | |
| **Idara ya Utawala na Uendeshaji** | 1,405,999 | 671,499 | 734,500 | - | - | - | 1,405,999 |

| Programu | Kazi za Kawaida | | | | Kazi za Maendeleo | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Jumla** | **Mishahar a** | **Matumizi Mengineyo** | **SMZ** | **Wahisani** | **Jumla Maendeleo** | **Jumla Kuu** |
| **Idara ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti** | 340,416 | 153,016 | 187,400 | - | - | - | 340,416 |
| **Ofisi Kuu Pemba** | 1,022,286 | 563,086 | 459,200 | - | - | - | 1,022,286 |
| Jumla ya Progamu ya Uendeshaji na Uratibu wa OMKR | **2,768,700** | **1,387,600** | **1,381,100** | **-** | **-** | **-** | **2,768,700** |
| **Jumla Fungu B01-F** | **4,395,815** | **2,348,245** | **2,247,570** | **3,500,000** | **1,451011** | **4,951,011** | **9,546,827** |
| Programu Kuu ya Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Kwanza wa Rais | | | | | | | |
| Ofisi ya Faragha ya Makamu wa Kwanza wa Rais | **1,199,685** | **625,155** | **574,530** | **-** | **-** | **-** | **1,199,685** |
| Jumla Fungu B01+Faragha | **5,795,500** | **2,973,400,** | **2,822,100** | **3,500,000** | **1,451011** | **4,951,011** | **10,746,511** |
| Programu Kuu ya Usimamizi wa Mazingira | | | | | | | |

| Programu | Kazi za Kawaida | | | | Kazi za Maendeleo | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Jumla** | **Mishahara** | **Matumizi Mengineyo** | **SMZ** | **Wahisani** | **Jumla Maendeleo** | **Jumla Kuu** |
| Mamalaka ya Usimamizi wa Mazingira | **1,574,000** | **1,030,800** | **543,200** | **-** | **-** | **-** | **1,574,000** |
| Progrmu Kuu ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya | | | | | | | |
| Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya | **1,747,685** | **862,508** | **885,177** | **1,500,000** | **-** | **1,500,000** | **3,247,685** |
| Progrmu kuu ya Kuratibu Muitiko wa Taifa wa UKIMWI | | | | | | | |
| Tume ya UKIMWI | **1,210,233** | **666,100** | **544,133** | **-** | **-** | **-** | **1,210,233** |
| **Jumla Taasisi za OMKR** | **4,531,918** | **2,559,408** | **1,972,510** | **1,500,000** | **-** | **-** | **6,031,918** |
| **JUMLA KUU** | **10,127,618** | **5,532,808** | **4,794,610** | **5,000,000** | **1,451,011** | **6,451,011** | **16,778,429** |

**Kiambatanisho nam. 3: Makusanyo ya Mapato kwa Julai-Machi 2022/2023 na Makadirio ya 2023/2024**

| Kifungu | Idara /Taasisi | Makadirio ya Mwaka 2022/2023 | Makadirio Jul – Machi 2022/2023 | Makusanyo Halisi | % ya mwaka | Makadirio 2023/2024 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **B04** | **B01 Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira** | 300,000,000 | 224,500,000 | 242,975,400 | 81 | 574,100,000 |

## Kiambatanisho nam. 4: Fedha za Miradi ya Mazingira

| Jina la Mradi | Chanzo cha fedha | Iliyopangwa | Iliyotumika | Makadirio kwa mwaka 2023/2024 |
|---|---|---|---|---|
| Kuirithisha Zanzibar ya Kijani | SMZ | 1,100,000,000 | - | 1,500,000,000 |
| Kuendeleza maeneo yaliyoharibika kimazingira | SMZ | 3,400,000,000 | - | 2,000,000,000 |
| Ukuzaji wa Wigo na Kuongeza kiwango cha Ufanisi wa Mfumo wa kusafisha maji machafu | UNEP | | 89,860,024 | 192,244,688 |
| Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa kutumia Mfumo wa Ikolojia Vijijini (EBARR) | UNEP | | 253,081,120 | 234,417,000 |

| Jina la Mradi | Chanzo cha fedha | Iliyopangwa | Iliyotumika | Makadirio kwa mwaka 2023/2024 |
|---|---|---|---|---|
| Uimarishaji wa Jamii na Usimamizi Endelevu wa Ikolojia na Shughuli za Kujipatia Kipato kwa Wavuvi Wadogo katika eneo la Hifadhi la Mkondo wa Pemba (PECCA) | UNEP | 318,616,700 | 41,285,400 | 249,829,200 |
| Kuimarisha Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa jamii za Pwani ya Zanzibar | Adaptation Fund | 796,030,163 | 145,618,058 | 774,520,500 |
| Ujenzi wa Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia – Kidimni | SMZ | 3,637,825,000 | 700,000,000 | 1,500,000,000 |

**Kiambatanisho 5: Maeneo ya Kimazingira na Mashimo yaliyokaguliwa**

| Jina la Mkoa/Wilaya | Maeneo | Mashimo |
|---|---|---|
| **Mkoa wa Mjini Magharibi** | | |
| Wilaya ya Mjini | 6 | |
| Wilaya ya Magharibi ‘A’ | 6 | |
| Wilaya ya Magharibi ‘B’ | 8 | |
| **Jumla 1** | **20** | |
| **Mkoa wa Kaskazini** | | |
| Wilaya ya Kaskazini ‘A’ | 12 | |
| Wilaya ya Kaskazini ‘B’ | 1 | 34 |
| **Jumla 2** | **13** | **34** |
| **Mkoa wa Kusini** | | |
| Wilaya ya Kusini | 17 | 18 |
| Wilaya ya Kati | 8 | |
| **Jumla 3** | **25** | **18** |

| Jina la Mkoa/Wilaya | Maeneo | Mashimo |
|---|---|---|
| **Jumla Unguja** | **58** | **52** |
| **Mkoa Wa Kusini Pemba** | | |
| Wilaya ya Mkoani | 9 | 13 |
| Wilaya ya Chake Chake | 12 | 18 |
| **Jumla 4** | **21** | **31** |
| **Mkoa wa Kaskazini Pemba** | | |
| Wilaya ya Wete | 8 | 8 |
| Wilaya ya Micheweni | 5 | 15 |
| **Jumla 5** | **13** | **23** |
| **Jumla Pemba** | **34** | **54** |
| **Jumla Kuu (Unguja + Pemba)** | **92** | **106** |

## Kiambatanisho nam. 6 Idadi ya Watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais

| Viwango vya Elimu | Sdt 1 - F.IV | | Cheti | | Stashahada | | Stashahada ya Juu | | Shahada ya Kwanza | | Stashahada ya Uzamili | | Shahada ya Uzamili | | Shahada ya Uzamivu | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | ***M*** | ***F*** | ***M*** | ***F*** | ***M*** | ***F*** | ***M*** | ***F*** | ***M*** | ***F*** | ***M*** | ***F*** | ***M*** | ***F*** | ***M*** | ***F*** | |
| **Idara ya Utumishi na Uendeshaji** | 9 | 5 | 1 | 1 | 2 | 10 | 0 | 0 | 5 | 3 | 0 | 0 | 4 | 2 | 1 | 1 | 43 |
| **Idara ya Mipango, Sera na Utafiti** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 2 | 1 | 0 | 2 | 2 | 0 | 0 | 8 |
| **Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu** | 7 | 7 | 0 | 0 | 5 | 7 | 1 | 0 | 11 | 19 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 59 |
| **Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu Pemba** | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 6 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 9 |
| **Idaara ya Faragha Pemba** | 3 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 6 |

| Viwango vya Elimu | Sdt 1 - F.IV | | Cheti | | Stashahada | | Stashahada ya Juu | | Shahada ya Kwanza | | Stashahada ya Uzamili | | Shahada ya Uzamili | | Shahada ya Uzamivu | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | ***M*** | ***F*** | ***M*** | ***F*** | ***M*** | ***F*** | ***M*** | ***F*** | ***M*** | ***F*** | ***M*** | ***F*** | ***M*** | ***F*** | ***M*** | ***F*** | |
| **Idaara ya Faragha Unguja** | 0 | 1 | 2 | 1 | 2 | 1 | 0 | 0 | 3 | 1 | 0 | 0 | 3 | 0 | 1 | 0 | 15 |
| **Idara ya Mazingira (Unguja)** | 4 | 3 | 0 | 2 | 4 | 0 | 0 | 1 | 8 | 3 | 0 | 0 | 5 | 3 | 1 | 0 | 34 |
| **Idara ya Mazingira (Pemba)** | 5 | 3 | 0 | 0 | 2 | 5 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 19 |
| **Mamlaka ya Mazingira (Unguja)** | 10 | 4 | 4 | 7 | 2 | 5 | 0 | 0 | 6 | 6 | 1 | 0 | 6 | 7 | 0 | 0 | 58 |
| **Mamlaka ya Mazingira (Pemba)** | 9 | 0 | 2 | 0 | 3 | 3 | 1 | 0 | 3 | 1 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 24 |
| **Tume ya UKIMWI (Unguja)** | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 6 | 1 | 0 | 2 | 6 | 0 | 1 | 3 | 4 | 0 | 0 | 24 |

| Viwango vya Elimu | Sdt 1 - F.IV | | Cheti | | Stashahada | | Stashahada ya Juu | | Shahada ya Kwanza | | Stashahada ya Uzamili | | Shahada ya Uzamili | | Shahada ya Uzamivu | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | *M* | *F* | *M* | *F* | *M* | *F* | *M* | *F* | *M* | *F* | *M* | *F* | *M* | *F* | *M* | *F* | |
| **Tume ya UKIMWI (Pemba)** | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 7 |
| **Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (Unguja)** | 8 | 0 | 3 | 2 | 3 | 4 | 0 | 0 | 5 | 9 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 34 |
| **Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (Pemba)** | 2 | 1 | 3 | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 4 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 15 |
| **Ofisi Kuu Pemba** | 2 | 2 | 0 | 0 | 1 | 4 | 0 | 0 | 4 | 1 | 0 | 0 | 1 | | 0 | 0 | 15 |
| **Jumla** | **59** | **28** | **15** | **15** | **30** | **48** | **4** | **1** | **57** | **58** | **3** | **1** | **30** | **18** | **4** | **1** | **372** |

**Kiambanisho nam. 7 Idadi ya Visaidizi Vilivyogaiwa**

| **Wilaya** | **Aina ya Vifaa Saidizi.** | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | ***Viti vya magurudumu mawili*** | ***Fimbo nyeupe*** | ***Bakora za kutembelea*** | ***Magongo ya Mkononi*** | ***Vigari vya WWU*** |
| 1. MKOANI | 40 | 12 | 24 | 12 | 13 |
| 2. CHAKECHAKE | 18 | 25 | 17 | 18 | 17 |
| 3. WETE | 19 | 16 | 12 | 23 | 17 |
| 4. MICHEWENI | 29 | 15 | 22 | 22 | 12 |
| 5. KUSINI UNGUJA | 14 | 12 | 18 | 17 | 12 |
| 6. KATI | 19 | 10 | 16 | 19 | 11 |

| **Wilaya** | **Aina ya Vifaa Saidizi.** | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | ***Viti vya magurudumu mawili*** | ***Fimbo nyeupe*** | ***Bakora za kutembelea*** | ***Magongo ya Mkononi*** | ***Vigari vya WWU*** |
| 7. MJINI | 17 | 16 | 10 | 10 | 3 |
| 8. KASKAZINI A | 11 | 17 | 8 | 20 | 12 |
| 9. KASKAZINI B | 15 | 10 | 13 | 16 | 4 |
| 10. MAGHARIBI A | 12 | 10 | 13 | 12 | 10 |
| 11. MAGHARIBI B | 12 | 20 | 16 | 13 | 21 |
| **Jumla** | **206** | **163** | **169** | **182** | **132** |